

CARDINAL RUGAMBWA MEMORIAL COLLEGE (CARUMCO)
BUKOBIA CATHOLIC DIOCESE

P.O. Box 1830,

Bukoba, Tanzania



Mob: +255 784887803
+255 714887803
+255 755915449

E-mail: info@carumco.ac.tz
rugambwacardinal9@gmail.com

Website: www.carumco.ac.tz

KUMB NA: CARUMCO/ADO/VOL 01/2023/2024

Mpendwa

**YAH: FOMU YA MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MASOMO KATIKA CHUO CHA
KUMBUKUMBU YA KARDINALI RUGAMBWA (CARUMCO)**

1. Hongera umechaguliwa kujiunga na chuo cha Cardinal Rugambwa Memorial College (CARUMCO) kwa ngazi ya Stashahada (Diploma). Kwa muhitimu wa kidato cha nne (4) kozi yako ni ya miaka mitatu (3) yaani Certificate mwaka 1 na Diploma miaka (2). Kwa muhitimu wa kidato cha sita kozi yako ni ya miaka miwili (2) tu. Hivyo tunakupatia fomu hii ili uanze maandalizi mapema.
2. Chuo cha CARUMCO kinapatikana **eneo la Nkindo - Itahwa, umbali wa Kilometa 6** kutoka stendi ya Mabasi ya Bukoba Mjini barabara ya kuelekea Muleba. Ukipanda gari (Daladala) nauli ni **Tsh. 1,000/=** tu na ukipanda pikipiki (Bodaboda) nauli ni **Tsh. 2,500/=** Kwa wanaotokea Muleba kuja Bukoba wanashuka Chuoni CARUMCO - Nkindo moja kwa moja.
3. **Tarehe ya kuwasili kwa ajili ya kufanya Usajili/Udahili.**
Unatakiwa kuwasili chuoni tarehe **20/07/2023** kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi saa 12:00 jioni ili kuanza kozi ya **KOMPUTA NA KINGEREZA** ambayo ni **OFA** kwa wanafunzi wote wataochaguliwa kujiunga na chuo chetu. Mwanafunzi atakaye jiunga na kozi hii atalipia gharama ya **chakula tu Tsh 100,000/=**.

Aidha, masomo rasmi ya ngazi ya cheti na diploma yataanza rasmi baada ya kozi hii fupi ya kingereza na komputa.

4. Mahitaji kwa ajili ya usajili.

Wanachuo wote waliochaguliwa watasajiliwa baada ya kukamilisha yafuatayo:

A. Malipo ya Ada.

- i. Baada ya kufanya malipo wasilisha risiti au stakabadhi ya malipo chuoni. Ikumbukwe kwamba, chuo hakitapokea malipo yoyote kwa hundi na taslimu.
- ii. Ada ikishalipwa, haitarudishwa kwa mwanachuo atakayeamua kwa hiari yake ama kuacha masomo yake au kuondoka chuoni.
- iii. Ufuatao ni mchanganuo wa Ada na malipo mengine katika jedwali hapa chini.

NB:Malipo haya yanalipwa kwa(AWAMU NNE) kama inavyoonekana katika ukurasa wa mwisho (**namba.8**) katika fomu hii.

NGAZI YA CHETI (NTA LEVEL 4)			
	Vitu vinavyohitajika	Wanachuo wa Tanzania	Wanachuo wa Kimataifa
		TZS	USD
1	Ada	850,000.00	400.00
2	Gharama za Utawala		
	Mitihani	50,000.00	25.00
	Kitambulisho	10,000.00	5.00
	Mazoezi kwa Vitendo (Field Assessment)	30,000.00	15.00
	Umoja wa wanachuo (CARUMCOSO)	10,000.00	5.00
	Udhibiti Ubora(NACTE)	20,000.00	10.00
	Capitation fees	50,000.00	25.00
	Provisional Results.	10,000.00	5.00
	Jumla	1,030,000.00	490.00

Jendwali na. 1

DIPLOMA			
	Vitu vinavyohitajika	Wanachuo wa Tanzania	Wanachuo wa Kimataifa
		TZS	USD
1	Ada	960,000.00	457.00
2	Gharama za Utawala		
	Mitihani	50,000.00	25.00
	Kitambulisho	10,000.00	5.00
	Mazoezi kwa Vitendo (Field Assessment)	30,000.00	15.00
	Umoja wa wanachuo (CARUMCOSO)	10,000.00	5.00
	Udhibiti Ubora(NACTE)	20,000.00	10.00
	Capitation fees	50,000.00	25.00
	Provisional Results.	10,000.00	5.00
	Jumla	1,140,000.00	547.00

Jedwali na. 2

Fedha zote hizi zilipwe kupitia **Benki ya MKOMBOZI**

BENKI YA MKOMBOZI - BUKOBA BRANCH

Jina la Akaunti: CARUMCO TUITION FEE ACCOUNT

Akaunti Namba 00611512222602

B. Nyaraka kwa ajili ya usajili.

- i. Mwanachuo atatakiwa kuleta nyaraka za vyeti halisi(original copies) vya kidato cha nne/kidato cha sita na cheti cha kuzaliwa(birth certificate). Kwa wale wenye Astashahada yaani NTA Level 4, wawasilishe cheti halisi katika ngazi hiyo ili kuhakiki uhalali wa sifa za kujiunga na ngazi ya Stashahada (diploma). Tunaomba kukutaarifu kuwa, Nakala za vyeti zilizo rudufiwa (photocopies), matokeo yaliyopakuliwa kutoka kwenye mtandao, faksi na matokeo yaliyoidhinishwa HAYATAKUBALIWA.
- ii. Mwanachuo anatakiwa kuwasilisha fomu ya vipimo vya kitabibu (medical examination report) kuthibitishwa na Daktari anayetambulika kisheria. Fomu kwa ajili ya vipimo imeambatanishwa nyuma ya fomu hii(**Ukurasa na.7**).

- iii. Wasilisha nakala halisi ya malipo ya benki (**original /pay in slip**) bank slip.
Hakikisha unabaki na nakala ya malipo.
- iv. Wasilisha picha mbili za rangi(**colored passport size photo**)

5. Chakula na Malazi

i. Chakula:

Wanachuo watakaoishi hosteli za chuo, watapata huduma zote za chakula chuoni. Kila mwanachuo atatakiwa kulipa **Tsh. 700,000/-** tu ikijumuisha Gharama za Hosteli na Chakula kama inavyoonekana katika jedwali namba tatu hapa chini. Endapo atahitaji kulala nje ya Chuo lakini chakula akipate Chuoni, atalipa **Tsh. 550,000/=** kwa mwaka.

CHAKULA NA MALAZI			
	Mahitaji	Watanzania	Wanachuo wa Kimataifa
		TZS	USD
1	Hosteli	200,000.00	120
2	Chakula	500,000.00	215
	Jumla	700,000.00	335

Jedwali na. 3

ii. Malazi

Kwa upande wa Malazi, mwanachuo atatakiwa kuja na Blanketi, mashuka zaidi ya mawili rangi yoyote, chandarua nyeupe, Beseni na Ndoo kwa ajili ya matumizi yake ya bwenini.

Godoro na kitanda atavikuta chuoni.

- **Mwanachuo asilete SANDUKU LA CHUMA au SANDUKU LA MBAO chuoni.**

NB: Gharama za chakula na malazi zitawahusu wanachuo watakaoishi Hosteli za chuo tu.(In Campus students only).

Fedha zote za Chakula na Malazi zilipwe kwenye akaunti ifuatayo:

**Benki ya MKOMBOZI:
Jina la Akaunti: CARUMCO SUSTAINABILITY ACCOUNT.
Akaunti Na. 00611512222601**

JUMLA YA MALIPO KWA WANACHUO WA BWENI NA KUTWA

	Vitu vinavyohitajika	Hosteli (In Campus)		Kutwa (Off Campus)	
		TZS	USD	TZS	USD
1	Cheti(Astashahada)	1,730,000.00	742	1,030,400.00	442
2	Diploma(Stashahada)	1,840,000.00	789	1,140,000.00	489

Jedwali na. 4

6. Vitabu na Machapisho.

Mwanachuo anatakiwa kufanya jitihada na mipango binafsi ya fedha kwa ajili ya kununua vitabu vyake binafsi, kufanya machapisho ya kazi na mazoezi mbalimbali ya walimu, kuandaa mrejesho wa mazoezi kwa vitendo (field attachment) na mahitaji mengine binafsi.

7. Nidhamu na Mavazi

(a) Nidhamu

Kila mwanachuo atatakiwa kuwa na tabia nzuri na kuhakikisha anaitunza na kuilinda heshima yake mwenyewe, ya wenzake pamoja na heshima ya chuo kwa ujumla huku akizingitia sheria na taratibu za chuo.

(b) Mavazi

Mwanachuo atatakiwa kuvaa mavazi ya heshima muda wote kama yalivyothibitishwa na kuidhinishwa na baraza la chuo (College Council).

Kwa kuzingatia heshima na maadili ya chuo chetu, wanachuo wote watatakiwa kuonekana katika mavazi maalumu ya chuo kama ifuatavyo

- i. Mwanachuo anapaswa kuja na fedha **kiasi cha shilingi laki moja (100,000/=)** wakati wa kuwasili chuoni kwa ajili ya **sare za chuo (Suti na T-shirts)**.
- ii. Mwanachuo alete Shati nyeupe mbili mikono mirefu, Tai nyekundu 1, viatu vyeusi vya ngozi vya kufunika visivyo kuwa na kisigino kirefu na soksi.
- iii. Mwanachuo anapaswa kuja na **nguo za nyumbani ambazo zinazidi magoti na zisizoonyesha maungo ya ndani**
- iv. Mwanachuo aje na Tracksuti moja (1) rangi ya Bluu pamoja na viatu vya michezo.

(c) Afya

Mwanachuo anapaswa kuja na **Tsh. 50,400/=** kwa ajili ya Bima ya Afya (NHIF)

8. Kuabudu.

CARUMCO inatambua haki ya mtu binafsi ya kuabudu. Hivyo, mwanachuo anashauriwa kutumia muda wake vizuri kutafuta huduma za kiroho zilizomo ndani au nje ya chuo bila kuingilia au kuathili shughuli zake za kitaaluma. Chuo kitasimamia imani ya wanachuo wote kupitia kwa mshauri wa wanachuo kiroho (chaplain).

Madhehebu ya kikristu wajitahidi kuwa na vitabu vya sala mbalimbali, Rozari na Biblia. Waislamu waje na Kuruwani zao.

KARIBU SANA



Ms. Abela Rwela

Afisa Usajili-CARUMCO



CARDINAL RUGAMBWA MEMORIAL COLLEGE (CARUMCO)
BUKOKA CATHOLIC DIOCESE

P.O. Box 1830,

Bukoba, Tanzania



Mob: +255 784887803
+255 714887803
+255 755915449

E-mail: info@carumco.ac.tz
rugambwacardinal9@gmail.com

Website: www.carumco.ac.tz



REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

SURNAME _____ OTHER NAMES _____
AGE _____ SEX _____
MARITAL STATUS _____ CITIZENSHIP _____

Please examine the above named as to his/her fitness for admission to the institute as a full time student.

MEDICAL CERTIFICATE

State normal/not normal

- | | |
|-----------------------------------|-------|
| (i) a) Eye, nose and throat: | _____ |
| b) Asthma: | _____ |
| c) Hearing: | _____ |
| d) Limbs: | _____ |
| e) Heart Disease: | _____ |
| f) Sick cell: | _____ |
| g) Epilepsy: | _____ |
| (ii) HIV: | _____ |
| (iii) Pregnancy: | _____ |
| (iv) Blood Sugar: | _____ |
| (v) Blood Group and HB: | _____ |
| (vi) Blood Pressure (BP): | _____ |
| (vii) Kidney and Urinary Disease: | _____ |
| (viii) Diabetes and Hypertension: | _____ |
| (ix) Ulcers: | _____ |
| (x) Others: | _____ |

I have examined the above named and consider that he/she is physically fit/ not fit for an intensive course of studies. (Delete whichever is not relevant)

Name of Medical Officer _____

Signature _____

Date _____

Official Stamp:

MODE OF PAYMENT (AWAMU ZA MALIPO)

FEE STRUCTURE AND INSTALLMENTS OF PAYMENTS FOR THE ACADEMIC YEAR 2023/24

BASIC TECHNICIAN CERTIFICATE (NTA 4)

FEE STRUCTURE:

NO.	ITEMS	IN CAMPUS			OFF CAMPUS		
		1st SEM	2nd SEM	TOTAL/YEAR	1st SEM	2nd SEM	TOTAL/YEAR
1	TUITION FEE	450,000.00	400,000.00	850,000.00	450,000.00	400,000.00	850,000.00
2	EXAMINATION FEE	50,000.00		50,000.00	50,000.00		50,000.00
4	CAPITATION FEE	50,000.00		50,000.00	50,000.00		50,000.00
5	NACTE Q/A FEE	20,000.00		20,000.00	20,000.00		20,000.00
6	CARUMCOSO	10,000.00		10,000.00	10,000.00		10,000.00
7	IDENTITY CARD	10,000.00		10,000.00	10,000.00		10,000.00
8	FIELD ASSESMENT		30,000.00	30,000.00		30,000.00	30,000.00
9	PROVISION RESULTS	10,000.00		10,000.00	10,000.00		10,000.00
10	ACCOMODATION	120,000.00	80,000.00	200,000.00			
11	MEAL	250,000.00	250,000.00	500,000.00			
	TOTAL	970,000.00	760,000.00	1,730,000.00	600,000.00	430,000.00	1,030,000.00

INSTALLMENTS:

IN CAMPUS				OFF CAMPUS			
1 Installment	2 Installment	3 Installment	4 Installment	1 Installment	2 Installment	3 Installment	4 Installment
Awamu ya 1	Awamu ya 2	Awamu ya 3	Awamu ya 4	Awamu ya 1	Awamu ya 2	Awamu ya 3	Awamu ya 4
OCTOBER	JANUARY	MARCH	JUNE	OCTOBER	JANUARY	MARCH	JUNE
560,000/=	410,000/=	540,000/=	220,000/=	400,000/=	200,000/=	280,000/=	150,000/=

MODE OF PAYMENT (AWAMU ZA MALIPO)

FEE STRUCTURE AND INSTALLMENTS OF PAYMENTS FOR THE ACADEMIC YEAR 2023/24 DIPLOMA

FEE STRUCTURE

NO.	ITEMS	IN CAMPUS			OFF CAMPUS		
		1st SEM	2nd SEM	TOTAL/YEAR	1st SEM	2nd SEM	TOTAL/YEAR
1	TUITION FEE	460,000.00	500,000.00	960,000.00	460,000.00	500,000.00	960,000.00
2	EXAMINATION FEE	50,000.00		50,000.00	50,000.00		50,000.00
4	CAPITATION FEE	50,000.00		50,000.00	50,000.00		50,000.00
5	NACTE Q/A FEE	20,000.00		20,000.00	20,000.00		20,000.00
6	CARUMCOSO	10,000.00		10,000.00	10,000.00		10,000.00
7	IDENTITY CARD	10,000.00		10,000.00	10,000.00		10,000.00
8	FIELD ASSESMENT		30,000.00	30,000.00		30,000.00	30,000.00
9	PROVISION RESULTS	10,000.00		10,000.00	10,000.00		10,000.00
10	ACCOMODATION	120,000.00	80,000.00	200,000.00			
11	MEAL	250,000.00	250,000.00	500,000.00			
	TOTAL	980,000.00	860,000.00	1,840,000.00	610,000.00	530,000.00	1,140,000.00

INSTALLMENTS:

IN CAMPUS				OFF CAMPUS			
1 Installment	2 Installment	3 Installment	4 Installment	1 Installment	2 Installment	3 Installment	4 Installment
Awamu ya 1	Awamu ya 2	Awamu ya 3	Awamu ya 4	Awamu ya 1	Awamu ya 2	Awamu ya 3	Awamu ya 4
OCTOBER	JANUARY	MARCH	JUNE	OCTOBER	JANUARY	MARCH	JUNE
570,000/=	410,000/=	540,000/=	320,000/=	400,000/=	210,000/=	380,000/=	150,000/=